

**HALMASHAURI YA WILAYA YA UKEREWE  
MKOA WA MWANZA**

Simu+255732981174/+255737178220

Fax: +255732981174/+255282515056

Email:ps@ukerewedc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W),

S.L.P. 41,  
NANSIO/UKEREWE

**TANGAZO**

22/01/2018

**UJENZI WA MAJENGO MBALIMBALI YA KUTOLEA HUDUMA KATIKA KITUO CHA AFYA  
BWISYA.**

Husika na somo tajwa hapo juu.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kupitia Serikali ya Denmark imetoa kiasi cha Tshs 400,000,000/= Tarehe 20/12/2017 siku ya Jumatano kwa ajili ya kufanya ujenzi wa majengo mapya ya kutolea huduma ili kukifanya kituo hicho kiweze kutoa huduma za upasuaji kwa akina mama wajawazito watakaoshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida.

Fedha hizo tayari zimekwisha kuingizwa katika akaunti za Halmashauri na hivyo zinatakiwa zianze kutumika. Maeneo/ majengo yanayokusudiwa kujengwa ni yafuatayo:-

1. Jengo la Upasuaji.
2. Wodi ya wakina mama wajawazito ( maternity ward)
3. Jengo la maabara.
4. Jengo la Kuhifadhia maiti. (Mortuary).
5. Ujenzi wa matanki ya kuhifadhia maji ya mvua pamoja na miundombinu yake.
6. Kichomea taka
7. Shimo la kutupia kondo la nyuma
8. Nyumba ya mtumishi

Mradi huu unatakiwa kutekelezwa na kukamilika kwa muda wa wiki 16. utekelezaji ambayo ni April 2018.

Mradi huu utakelezwa kata ya Bwisya hivyo natoa rai kwa uongozi wa kata pamoja na wananchi kutoa ushirikiano katika kukamilisha mradi huu utakao kuwa wa manufaa kwa wananchi.

*Bhati*

FRANK S. BAHATI  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
UKEREWE

**MPURUGENZI MTENDAJI (W)  
UKEREWE**